Vita Ambayo Shetani Hatashinda
(The Battle Satan Could Not Win)

na

Alex Silvester

Vita Ambayo Shetani Hatashinda

(The Battle Satan Could Not Win)

na

Alex Silvester

Sept 3, 2016

Vita Ambayo Shetani Hatashinda

Ufu. 12:7-12

Ndugu ningependa kushiriki nanyi katika hili. Na kama Wakristo tunapaswa kulichunguza neno la Mungu ili kwamba likae kwa wingi ndani yetu.

"*Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, aaudanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye. Nikasikia sauti kuu mbinguni ikisema, sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku. Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. Kwa hiyo shangilieni, enyi mbingu, nanyi mkaao humo. Ole wa nchi na bahari! Kwa maana yule Ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa anawakati mchache tu.*" (Ufu. 12:7-12).

Inaweza kutokea katika kanisa kwamba wapo wale wanaotumiwa na Shetani ili wasababishe mgawanyiko miongoni mwa ndugu; na hivyo tunapata kwamba kanisa linagawanyika. Ndio maana Roho wa Bwana ni mwerevu na hivyo akatuandikia na kutuambia kwamba tuwaangalie wale wanaosababisha vita na mgawanyiko katika Kanisa la Bwana wetu. Wengi wanaweza kuinuka na kutudhihaki pale wanapoona kuna sababu. Tunaambiwa kuwaiga wale waliofanyika Wakristo na walikuwa na mifano mizuri, wanasemwa vizuri katika kazi ya Bwana, tunajifunza kutoka kwao na kufanya kama walivyofanya.

Mtume Paulo akiwa mmoja wa hawa watu, alipigana vita vilivyo vizuri na akakimbia mbio zilizo nzuri na tunaambiwa na Neno, kwamba Paulo alikuwa anasubiri ili apokee zawadi iliyowekwa sehemu ya juu mbinguni. "*Ndugu zangu mnifuate mimi mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfaano tuliowapa ninyi. Maana wengi huenenda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi, kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; mwisho wao ni uharibifu, Mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani.*" (Fil. 3:17-19). Agizo hili halijapewa kusanyiko moja tu, bali wamepewa

Makanisa yote ambayo yamefuata mfumo wa kuwa katika Rum. 16:16.

Shetani amekuwa akitunyemelea hata leo na kama haitoshi bado anawalazimisha watu wa kanisa la Bwana kukataa kilicho chema na kufuata kilicho kibaya. Hatupaswi kumruhusu kushinda kwa sababu alipo kuna wivu na ubinafsi, ndugu haya ni baadhi ya mambo yanayosababisha kanisa lisikuwe. Na kwa hili tunahitaji mafundisho mengi na kusoma neno la Mungu vyema. "*Maana hapo palipo wivu na ugomvi ndipo palipo machaafuko na kila tendo baya. Lakini hekima itokayo juu kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kussikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki.*" (Yak. 3:16-17). Kama Wakristo, mara nyingi tuna vikwazo vinavyosababishwa na Shetani na inapotokea tunamruhusu kutawala maisha yetu. Tunafahamu kwamba alitupwa chini kutoka mbinguni, alipotaka kuwa na mamlaka juu ya Mungu. Tena wengi wetu tunadhani ni werevu katika hatua kwamba tunakataa kufuata amri za Mungu. Hakuna aliyemwerevu kuliko Mungu na Mwana wake Yesu Kristo. "*N'nani aliye na hekima na ufahamu kwenu? Na aonyeshe kazi zake kwa mwenendo wake mzuri, katika upole na hekima. Lakini mkiwa na wivu wenye uchungu naa ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu wala msiseme uongo juu ya kweli. Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani.*" (Yak. 3:13-15). Wakristo wanapasswa kumkataa Shetani na kazi zake kwa sababu hazizai matunda, bali ya Mungu huzaa matunda. Wanadamu wanapenda njia ya mkato ambayo haiwezi kutufikisha mbinguni.

Vitu kama mgawanyiko husababisha kanisa kutokukua kwa sababu kila mmona haaongei kama neno linavyoongoza. Bwana wetu aliombea umoja ili kwamba ssote tuwe wamoja katika mwili wake na tunapokuwa na umoja tunapendana sisi kwa sisi, na kwa kufanya hivyo Shetani anaibika. Kuna baadhi wanaojali kila msshirika iwe nje ya nchi au Afrika Mashariki.

Mwisho, Mungu alimshinda Shetani alipokoswa uwezo, alipopoteza sehemu na alipopoteza nafasi ya kuwa mbinguni. Katika kifungu chetu cha maandiko Shetani anazungumziwa kama joka, nyoka, Ibilisi, Shetani, mdanganyifu au mshitaki. Na atatenda mabaya katika dunia, akijua kwamba ana muda mfupi na hii ndio maangamizi yake. Wazo ni nini? Wakati ndugu wanajaribu kupigana na kanisa, wanashindwa kutambua kuwa ni la Kristo na kwamba tunapaswa kufuata na kufanya mapenzi yake, bila kujali tuko katika hali gani. Na hii inajumuisha amri yake ya kupendana sisi kwa sisi. Ibilisi alijaribu kupigana na Kristo na akapoteza. Na pia alijaribu kupigana na kanisa kwa ujumla na akapoteza. Hata

sisi yeyote atakaye jaribu kupigana na kanisa atapoteza na kutupwa nje ya kundi. Ushindi pekee wa Shetani utakuwa dhidi ya Mkristo mmojammoja waliomwachia Shetani Kristo na Kanisa. Pia na wale ambao hawajajitoa kwa ajili ya Kristo.

Bwana wetu mwema atusaidie kufikia mapenzi yake.

Sadat Silvester